# DC amwaga machozi akijitetea maadili

**Na Anastazia Anyimike, Dodoma**

MKUU wa Wilaya ya Tanganyika, Onesmo Buswelu ametoa machozi mbele ya Baraza la Maadili ya Viongozi wa Umma wakati akijitetea tuhuma za kukiuka maadili.

Buswelu alisema Dodoma jana kuwa si kawaida yake kutoa machozi na akadai kuwa tuhuma dhidi yake zimetengenezwa.

"Nisipowaambia haya hamtaelewa, naadhibiwa kwa sababu ya kumsaidia Rais Samia kufuatilia fedha anazozileta. Hata wakati naingilia kazi matumizi ya tofali zile mbovu sikujua kuwa ni za meya," alisema.

Buswelu alituhumiwa kutumia lugha za matusi na kutumia madaraka vibaya kwa kuwaweka watumishi mahabusu na awali alipokuwa akisomewa mashtaka alizikana.

"Sijatumia lugha chafu na za matusi kwa watumishi na watendaji, kazi za ukaguzi wa miradi sijazifanya nikiwa peke yangu nimezifanya nikiwa na viongozi wenzangu wa kamati ya usalama ya wilaya," alisema.

Buswelu alisema hakuwahi kutoa maelekezo moja kwa moja kwa watumishi bali kwa mkurugenzi na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) na hakuwahi kumpeleka mahabusu mtumishi au mtendaji yeyote.

Alitoa mfano kuwa katika mradi wa ujenzi wa Jengo la Wagonjwa Mahututi (ICU) baada ya kutoka kwenye kikao cha kusikiliza changamoto za watumishi wa sekta ya afya walipata taarifa za kintelijensia kuwa tofali zinazotumika hazina ubora.

"Halima aliyesema nimemtolea lugha ya matusi mume wake ni Meya wa Mpanda (hakumtaja jina) ndiye aliyehusika kuuza tofali zisizo na ubora na alikuwa akifanya ubadhirifu kwenye halmashauri na niliagiza mkurugenzi kupitia tenda ya chakula alichokuwa akiuza kwa bei kubwa na baadhi ya vyakula hakupeleka pamoja na kulipwa fedha," alisema Buswelu.

# Taasisi ya Kapuya yazuiwa nchini, yachunguzwa

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesitisha shughuli za shirika lisilo la kiserikali la Athuman Kapuya kote nchini na linachunguzwa.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dorothy Gwajima ameeleza kuwa shirika hilo limesajiliwa kisheria mwaka 2021.

Taarifa ya Dk Gwajima ilieleza kuwa malengo waliyotekeleza na kusababisha Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Paul Chacha kulifunga ni kinyume cha katiba waliyosajili na pia ni kinyume na sheria ya usajili wa mashirika yasiyo ya kiserikali.

"Ofisi ya msajili kupitia Bodi ya Uratibu wa mashirika hayo tayari imesimamisha utendaji kazi wa shirika hilo kote nchini kupisha uchunguzi na hatua zaidi. Baada ya uchunguzi kukamilika, wahusika wote watachukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa sheria," ilieleza taarifa hiyo jana.

Juzi Chacha alitangaza kuipiga marufuku taasisi hiyo kufanya kazi mkoani humo.

Alitangaza uamuzi huo alipokuwa akizungumza na wadau wa elimu katika kikao kilichofanyika ukumbi wa halmashauri ya wilaya hiyo.

Chacha alisema walikamata vitabu vyenye machapisho ya kufundisha na kuhamasisha vitendo vya mapenzi ya jinsi moja.

Alisema vitabu hivyo vilikuwa vikiandaliwa kusambazwa katika shule za msingi na sekondari wilayani Kaliua kupitia taasisi hiyo yenye makao yake makuu Dar es Salaam.

Chacha alisema kitendo hicho si cha kiungwana kwa watoto na akaamuru mratibu wa taasisi hiyo, Tabitha Kapuya akamatwe na kufunguliwa mashitaka kwa kusambaza na kushawishi vitendo vya mapenzi ya jinsi moja.

Chacha alimuagiza Katibu Tawala wa Mkoa wa Tabora, Dk John Mboya aandike barua kwa uongozi wa serikali mkoani Dar es Salaam kuijulisha kuhusu taasisi hiyo ili isifanye kazi nchini.

Alisema taasisi hiyo imekuwa ikitoa misaada ya vitabu na kuvisambaza katika mikoa ya Tabora, Dar es Salaam na Zanzibar.


NA TANGAZO
DHARA

IPANY LIMITED, JEMBE NI JEMBE COMPANY
RAL COMPANY LIMITED, LYAMAKI LIMITED,
TED,PSALM AUCTION MART, HOLLYNESS &
SOLUTIONS. kwa idhini waliyopewa na PLATINUM
dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa
ana husika zitauzwa kwa njia ya mnada. Mnada utafanyika
. Muda ni kuanzia saa Tatu kamili asubuhi na kuendelea

| NA ILIPO | KAMPUNI INAYO HUSIKA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|
| GORO | JEMBE NI JEMBE COMPANY LTD | 20-06-2024 |
| SALAAM | PSALM AUCTION MART | 20-06-2024 |
| SALAAM | CITY LINK INVESTMENT LIMITED | 20-06-2024 |
| SALAAM | CITY LINK INVESTMENT LIMITED | 20-06-2024 |
| A | GORETHFLUX GENERAL CO LTD | 20-06-2024 |
| SALAAM | CITY LINK INVESTMENT LIMITED | 20-06-2024 |
| SALAAM | CITY LINK INVESTMENT LIMITED | 20-06-2024 |
| SALAAM | WORK ETHIC COMPANY LIMITED | 20-06-2024 |
| A | CITY LINK INVESTMENT LIMITED | 20-06-2024 |
| SALAAM | CITY LINK INVESTMENT LIMITED | 20-06-2024 |
| SALAAM | PSALM AUCTION MART | 20-06-2024 |
| SALAAM | PSALM AUCTION MART | 20-06-2024 |
| SALAAM | PSALM AUCTION MART | 20-06-2024 |
| | CITY LINK INVESTMENT LIMITED | 20-06-2024 |
| SALAAM | GORETHFLUX GENERAL COLTD | 20-06-2024 |
| SALAAM | PSALM AUCTION MART | 20-06-2024 |
| ORO | LYAMAKI LIMITED | 20-06-2024 |
| SALAAM | CITY LINK INVESTMENT LIMITED | 20-06-2024 |
| IA | HOLLYNESS & RESPISHERS CO LTD | 20-06-2024 |
| SALAAM | WANGI AUCTION MART | 20-06-2024 |
| ZA | WANGI AUCTION MART | 20-06-2024 |
| SALAAM | HOLLYNESS & RESPISHERS CO LTD | 20-06-2024 |
| ZA | WANGI AUCTION MART | 13-06-2024 |
| SALAAM | JEMBE NI JEMBE COMPANY LTD | 13-06-2024 |
| ALI A | HOLLYNESS & RESPISHERS CO LTD | 13-06-2024 |
| SALAAM | CITY LINK INVESTMENT LIMITED | 13-06-2024 |

ya nyundo ya dalali kutua na salio la 75% liwe limelipwa

atarejeshwa na mnada utarudiwa.
va manunuzi zitakua juu ya mnunuzi. Kampuni itasaidia

7200064

ORD00018415